Tutabandika wewe wakati unakufa. Present MPs walioko sasa walijibandika mishahara mikuwa hiyo tite ya mhesimiwa waondolewe kwa sababu walikula pesa yetu na kujibandika. Wasiitwe waheshimiwa tena. Pengine waitwe waheshimiwa waporaji.

(Laughter)

By election iwe minimized. Kusiwe na by-election tena. Wewe ukitoroka chama ukienda chama kingine marufuku maisha yako hautakuwa mwanachama, nenda kabisa kabisa kabisa.

Kuna jambo la kusikitisha sana. Kuna hii ukinajisi mtoto mdogo kabisa unafungwa miaka kumi na mine. Hiyo haitoshi. Ufungwe miaka kumi na minee na uwe castrated within 24 hours. Ndiyo hiyo mambo hautarudia tena.

(Laughter)

Kwa maana ukitoka huko utakuja kurudia hiyo mambo ingine.

Kuhusu Kenyadtta Day, hii siku alijibandika yeye peke yake na alifungwa na kina Paul Ngei, Bildad Kagia, Ochieng' Oneko, Karumba, ibadilishwe na iitwe siku ya wapigania uhuru. Hiyo itolewe.

Siku ingine ambayo haina maana ni Moi Day. Hiyo weka siku ya Oppression day ya nyayo era. Pengine tutakumbuka na hiyo. Hiyo tutakumbuka vile tuliteswa wakati wa mwakenya. Pengine wale wengine hawakuwako watakuwa wataikumbuka.

Wakatibunge linavunjwa, maministers watoka kwenye viti kabisa sababu wakiwachiwa ofisi, watatumia mamlaka yao kuja kwa campaign na zile gari za serikali zote zirudishwe. Hata haifai waziri kupewa gari ya serikali. Wapewe allowance ya gari na there should be no ministerial car. Government cars should be very limited.

**Provincial Administration:** Kama Assistant Chief na Chief wanatoka kwa area hiyo, hata D.O. kama ni Division, huyo D.O atoke kwa hiyo division, awe ni mtu wa division hiyo. D.C awe anatoka Mwingi, awe ni mtu wa hapa Mwingi. Province awe anatoka kwa hiyo Province kwa maana sasa tunaona kutoka 1963 mpaka 1977 tulikuwa na maDC akina Koinange, Mahihu, Mburu, nini na kutoka 1978 mpaka sasa ma Kipkemboi, arap Chirchir, arap nini...

(Laughter)

Haifai. Ni lazima kila District iwe na District Commissioner kutoka kwa District hiyo. Hatutaki hii mambo ingine.

Vice-President achaguliwe na watu wote ili asiwe anahangaishwa. Tumekaa miezi kumi na mine hatuna Vice-President na kila mtu alikuwa anaangalia oh baba unaweza kunipatia. Hiyo ikome.

Utukufu, kuabudu mtu. Katiba iseme hakuna kuabudu mtu.

Delegations za kwenda kwa Rais, ati Wakamba wote wanang'arang'ara na yeye tu anang'aranga pekee yake sasa anasema Wakamba wote wanang'arang'ara. Hiyo ni mbaya sana na hii katiba .....

Parliament iwe na calender yake na isiwe iki-contriliwa na mtu mmoja.

Rais awe ni mtu wa kukaa kwa ofisi. Asiwe Field Officer wa kuzunguka, ana mangamanga huko kila wakati na ni lazima account safari zake zote za kwenda ng'ambo kwa sababu hiyo ni pesa za wananchi anatumia.

Ya mwisho chukua hii yangu yote weka kwa katiba.

(Applause)

Mna swali?

**Com. Bishop Njoroge:** Hapana.

**Joseph Kasina:** Kama hamuulizi swali, yangu ni sawa sawa.

**Com. Bishop Njoroge:** Umezungunza vizuri. Haya njoo hapa. Peter Mulavu. Unajua uzuri wa katiba hii ni kwamba kila mtu anaruhusiwa kusema anavyoongoswa kusema isipokuw amtu haruhusiwi kusema mabaya kwa mtu mwingine. Si ni ukweli?

**Peter Mulavu:** Preamble.

Judiciary be vetted by Parliament

General elections: Parliamentary and Civic elections be separated from Presidential elections.

**Jacob kitheka:** Sijui nizingumze kwa lugha gani...

**Com. Bishop Njoroge:** Unajua unapotezza wakati wako?

**Jacob Kitheka:** Okay. Wacha niende moja kwa moja.

Katika katiba mpya mwananchi apewe uwezo wa kuchukua hatua juu ya watu wafisadi. Kwa wakati huu tunawaona, wanaendelea ha hakuna kitu cha kufanya. Unaenda kwa Police hawafanyi chochote. Ningefikiria katiba inipe mimi uwezo wa kulazimisha OCS, OCPD kuchugua hatua na kama hachukui hatua, nimpeleke kotini alazimishe na court kuchukua hatua.

Namba mbili; katiba impe uwezo mwananchi, akikosewa na ofisa wa serikali, apelike yule ofisa amemkosea koti iliyo karibu. Siyo high court kama ilivyo sasa. Na asilazimishwe kumpeleka pamoja na Attorney General maana Attorney General amekuwa kizuizi cha kutetea mwananchi asiweze kudai haki yake.

Wengi tumeshtuka tukisikia ya kuwa Attorney General lazima umshtaki na huyu Assistant Chief ambaye amekuvunja mguu. Kwa hivyo katiba inipe uwezo niende court iliyokaribu nimshtaki, tukimbisane, kama alikuwa kazini serikali itamlipia, kama hakuwa kazini, atanilipa.

Katiba utoe uwezo kamili kwa mwananchi ambaye anachagua viongozi. Awe na uwezo wa kumwondoa kiongozi yeyote aliyechaguliwa akiwa na tabia mbaya au kama anashindwa na kazi yake. Hiyo ni kusema kwamba badala ya councilor kuniambia miaka tano hautanifanya chochote, akianza kunifanya namna hiyo, niwe na uwezo wa kumuondoa na kuweka mwingine. MP nimwondoe na kuweka mwignine, President nimwondoe na kuweka mwingine.

Katiba imeandikwa haki zetu. Haki zetu zipo lakini namna ya kuzidai hakuna. Katiba mpya ni lazima inionyeshe vipi nitazidai haki zangu. Kama ni kwenda kotini ndiyo nipewe haki zangu, nipewe uwezo wa kufanya hivyo maana zimeandikwa lakini namna ya kuzifikia hakuna.

Juu ya mambo ya mashamba. Cases za mashambal. Disputes; imegawanywa kwamba ukitaka kushtaki hii uende pale, ukitaka hii uende pale. Kama unaambiwa uende kwa Tribunal, unaende kwa Tribunal. Kama mwignine alivyosema hapa, haujaenda school hata siku moja, ukianza kuwaambia sheria haisemi hivi, wanakwambia usitufunze kazi yetu. Haukuenda course pahali popote lakini wameshajua.

Kwa hivyo katiba mpya impe mwananchi uhuru wa kupeleka kesi yake ya shamba pale atakavyo. Akitaka kuanzia kotini, aanzie kotini. Akitaka kwa Adjudication, aanzie huko. Akitaka kuanzia kwa Tribunal aanzie huko lakini asilamishwe kwenda ambako hakuchagua.

Katiba mpya; ningefikiria kwamba kuna wazee wanaitwa villege elders hawatambulikani serikalini. Mimi nafikiri hawa wazee ni wa maana sana na kwa values za kitamaduni, wangechukuliwa kwa njia fulani, wawe wanatambulikana.

Na ya mwisho ni juu ya Commission yenyewe. Mtaniruhusu macommissioner nusu dakika niseme kitu moja juu yenu. Na hiyo ni kwamba wakati tumlitufunza, mlizunguka mkitufunza mnatuambia ya kwamba haifai mtu kuchukua nafasi.... It is inhuman to



take advantage of a plight or poverty of a person in order to exploit that person.

Ninefikiria Commission mpya ambayo pengine itakuwa ndani ya katiba, wakati ujao ufanye kile inafunza. Wakati huu haikufanya. Mtaniwia radhi haikufanya kwa sababu watu wengine waliokuw awakifunza hapa wanaenda huo with empty stomachs wanarudi nayo na kwa sababu wanapenda kazi wanaendelea. Wanaendelea tu. Na mwalimu wangu Ronald Ngala aliniambia kitu kizito zaidi ni tumbo tupu.

Kwa hivyo wakati unatuma mtu, kwa upande wangu naona ni exploitation maana huyu maskini atafanya tu kwa shilingi mia tatu ambayo ndiyo transport yake, ndio...hakuna chakula. Ni transport na makaratasi ya kutangaza. Makaratasi ya kutangaza ni shilingi mia tatu. Kwa hivyo Commission vile inatufundisha haki za binadamu, nayo wakati inafanya kazi itunze haki za binadamu.

(Applause)

**Com. Bishop Njoroge:** Mzee kaa hapo tu. Umesema vizuri na mambo hayo umeyasema bila shaka mimi mitayapeleka katika Commission tukiwa na Commissioner mwenzangu. Lakini pia ningetaka kusema hivi; kile kiwango cha fedha, sisi kama Commission hatuna njia yoyote ya kupata fedha isipokuwa ile tunapewa na serikali. Na tukipewa hicho kiwango, ndicho tunapeana kwa hivyo jambo la kwanza tunahitaji kuomba ni kukiwa na Commission kama hii, kuwe na fedha ya kutosha ili kila mtu aweze kufanya hiyo kazi akiwa na kitu ya kumlipa. Kwa hivyo Commission inapeana kile ilicho nacho.

Kama hatuna, hatuwezi. Si ni ukweli? Kwa hivyo tuamini kwamba Commission Nyingine ipewe fedha ya kutosha ili wale wanafanya katika constituency na wao waweze kuangaliwa. Sawa?

**Jacob Kitheka:** Hiyo ni sawa nakubali lakini? Unaweza ku-compare tu vile ma-provider wanaishi na vile macommissioner wanaishi. Pengine macommissioner wanaweza wakakata ma corner corner zingine wakawapa hawa chakula. Kutuma mtu bila chakula ndiyo mimi nasungunzia kwamba ni natural injustice.

**Com. Bishop Njoroge:** Sawa. Hapo tumefahamu na mimi nilikuwa tu nikikuelezea. Asante.

**Com. Zein:** Asante kwa maoni yako na ikiwa una malalamishi ingine kuhusu Tume, tafadhali utuandikie, ili tuweze kuyafuutilizia. Asante.

**Com. Bishop Njoroge:** Haya tupate Peter Malavu.

**Peter Mulavu:** These views are from people of Mariakani sub-location.

**Com. Bishop Njoroge:** You were here.

**Peter Mulavu:** This is a different District.

**Com. Bishop Njoroge:** Can you just present the memorandum. Haiya. Mwanzia Musyoka. Na nignetaka kwa wakati huu ku-recognize the presence of the Minister who is the member of Parliament of this area. Karibu sana mheshimiwa na wakati unataka kuzungumza nitakupatia nafasi.

**Mwanzia Musyoka:** Asanteni sana MaCommissioner. Kwa jina naitwa Mwanzia Musyoka. Mimi ni mmoja wa wenye Organization ambayo inajiita Mwingi Human Rights and Civic Education Services na kwa niaba ya group hiyo, nina memorandum nataka kutoa sababu mambo ya kundi iliyo hapa ni mengi na siwezi kuyazugnumza yote mpaka dakika ya mwisho lakini kuna jambo ambalo ningetaka kuongea.

Jambo ambalo ningetaka kuliongea ni jambo ulinzi. Hili iwekwe katika katiba ya sasa kwa sababu ulinzi katika nchi hii ya Kenya una shida nyingi kwa sababu tunapoteza watu viongozi wakubwa, watu raia na wakikufa au wakiuawa na wengine, ukifuatilia jambo hilo unaona haiangaliwi kikamilifu.

Polisi wanaficha mambo fulani, idara inayohusika na upelezi nayo inashindwa kutekeleza wajibu ambayo imeripotiwa. Kwa hivyo katiba ya sasa wanagroup tunaomba iweke ulinzi kamilivu kwa mwananchi wa kawaida kwa sababu watu wengi wanakufa na wakifaukifuatilia kifo chake kutokana na kuuawa ama kupewa dawa, serikali inatatiza. Jambo hilo ndilo ningezungumzia. Nina maneno mengi ambayo ningetaka kuyapeana lakini sitaweza kwa sababu dakika ni chache.

**Com. Bishop Njoroge:** Asante sana. Hayo umeyasema tumeyapata na bila shaka yatafika mahali inahitajika. Unaweza kupeana memorandum yako hapo. Tupate Elizabeth Munyithia.

**Elizabeth Munyithia:** Thank you Commissioner. Mine is about Gender equality and I will emphasize on the nominating of the Councilors and MPs. Since we know that traditionally ladies are not supposed to lead men, I will propose that the ratio of nominated MPs and Councillor should be three to one. That is three ladies to one man so that we may win favour from the Constitution and also increase the number of ladies in Parliament as well as in top seats.

My second point concerns the Ministry of Education. I propose that the constitution should guarantee every mwananchi compulsory and free education from pre-unit to university. This is to curb the illiteracy in the Country. The issue of cost sharing should stop.

My third point also concerns the Ministry of Education. I propose that the ministry should train teachers whom it thinks it can employ so as to avoid inconveniences such as; The trainees spend a lot of money in college fees with a hope that after employment they will compensate for the money.

Secondly it affects the teachers or the student teachers psychologically and mentally if they are not employed.

My fourth point is about considering of age when employing government servants. I propose that the older ones should be employed first so as to avoid retiring early when someone has not saved anything to cater for the old age. Thank you.

**Com. Bishop Njoroge:** Thank you very much for those views. Mama njoo hapa. Njoo hapa mbele. Tunamwita Munyasia Musya.

**Munyasia Musya:** Thank you Commissiners. My na me is Munyasia Musya, am a civil servant, District Information officer, Mwingi.

My first view is that the Constitution should entrench the work of the media in it so that as in the case of a press council that is self-regulatory and also remove the shilling one million requirement for those people who want to invest in the media industry. I suggest that the members to this media council come from the parliament and other; the media houses, media owners, the civic society and any other relevant persons and these must be vetted by parliament.

Secondly, just like it goes like one-man one vote, so be it with one-man one job sothat this Country can share the limited resources and employment opportunities fairly.

Another point is that the people of Kenya should be given independence of freedom for regional self-determination in economic and social matters. The people of Mwingi for example, should be allowed to determine matter to do with their economic welfare. For example livestock, which is thse mainstay of this District, is still under developed and therefore if the people of Mwingi through their local authorities decide that it is to their best interest to develop this sector of the economy and propose to the central government that funding should be given, I believe whatever they suggest that whatever they suggest should be given as it is without any ratification or determination by officers sitting in Nairobi.

Another thing is that the Constitution of Kenya should define administrative units as well as parliamentary and civic represantation units so that there are not conflicts in this matter.

I also suggest that the salaries of members of parliament should be made unadmirable so as to ward off those greedy and selfish persons who want to take up this job for the monetary gain rather than service to the people.

The civil service should also be entrenched in the constitution so that a body or a commission even for example the existing civil service commission becomes independent in order to oversee the work and the interests of civil servants without undue interference from other arms of the government.

I also suggest that this constitution establish ministries and provide on how they shall be run so that one ministry or department does not seem to be subsidiary to others.

I also suggest that on the event of very fundamental issues that arise in parliament, that MPs vote, there should be consultation by all MPs with their relevant electorate on pertinent issues that arise in parliament. As of now, we know in so many areas where members of parliament sit in Nairobi and vote on very important matters pertaining to their people without any consultation.

It does not arise, I don't think it is good for MPs once they are elected to parliament to view themselves as if the voters have ceded their right to influence what MPs do in parliament. I think the electorate should have the authority to determine these issues and I suggest that barazas or other means like those be held in order to determine that.

The last point is that MPs should spend considerable time in the constituency to make themselves conversant with the problems affecting their people and the electorate be allowed to remove sitting MPs if found wanting in their jobs. Thank you.

**Com. Zein:** Mr. Musyoka you have proposed that we should have restrictions indicated in the constitution that we should reserve one job for one person. Is this in Public or in the Private sector or both?

**Munyasia Musya:** I suggest that it be in Public Service.

**Com. Zein:** Thank you. Please sign.

**Com. Bishop Njoroge:** Francis K. Mwikia? Catherine Kigonge? Mary M. Jacob?

**Mary Jacob:** Hamjamboni. Kwa majina naitwa Mary Jacob. Nataka kutoa maoni yangu kuhusu katiba.

Kwa maoni yangu nataka katiba ile tunaandika sasa, wanawake wawe na usawa na wanaume.

Ya pili ni uridhi wa mali. Twaomba mwanamke awe na uridhi ya mali yake na nina sababu. Jamii nyingi zimevunjika kwa sababu ya hiyo. Tukiona sasa kwa mfano mzee aende am mimi niende, wale ndugu za bwana wangu wanifukuze pamoja na

watoto wangu, tunaenda na tukija kotini hiyo mambo hatuanganiwi na mtu. Kwa hivyo tunaomba katiba ile iko iwe inaandikwa uridhi wa, kwa mfano, kama ni mali yetu na mzee, inaandikwa mali yangu na mzee, siyo mali ya mzee pekee yake.

Ya nne ni wasichana wetu. Pia wao wakatiwe kasehemu wanaweza kulima kwa sababu wasichana wetu siku hizi hawaolewi. Hayo ni maoni yangu.

Ingingine ni maoni ya kisomo. Watoto wetu wanasoma na hawapati kazi. Kwa hivyo naomba watoto wetu wakisoma wawe wanapata kazi. Asante sana.

**Com. Bishop Njoroge:** Asante sana mama kwa hayo maoni mazuri. David M. Kilonzo? Brian M. Maliti? Joseph M. Mwendwa? Mwanzia Kalebe? F.M. Ngindu? P.M. Syethoka? B.M. Kilonzo? D.K Mwaka? D. Maluki? Councillor B.M. Mutio?

**Benson Mukiti Mutio:** Asante sana bwana Commissioner. Majina yangu councilor Benson Mukiti Mutio kutoka kata ya Kakuyu.

Maoni yangu nitayasema kwa luga ya Kiswahili. Kwanza ningependekeza katiba mpya tuwe na President na makamu wake. Pia tuwe na waziri mkuu na Waziri mkuu na naibu wake na wawe wabunge.

Waziri mkuu kama inawezekana, awe ndiye mwenye mamlaka ya kuunda serikali au kuchagua baraza la mawaziri. Na awe na uwezo kamili wa kutunza nchi; yaani security na pia awe mwenye uwezo wa kuchagua ma- permanent secretary wanaoendesha serikali.

Pia ninapendekeza kuwa wale watakao tunukiwa vyeo vikuu kama vile ma-permanent secretary na pia mawaziri wawe watu ambao ni waaminifu kwa nchi. Na kama mtu amewahi kutajwa sehemu fulani kama mhusika wa mambo mabaya, jambo hili ichunguzwe hata na bunge na ikionekana kama kuna doa doa aulizwe ajiondoe kwa hayo mamlaka kwa sababu siyo mwaminifu kwa nchi yake.

Pia ningetaka nafasi zile kuu kama vile Police, maofisa wakuu wapatiwe mamlaka kupitia records zao nzuri ili tuwe na polisi wenye nidhamu ya hali ya juu ambao wanaweza kuchunguza makosa kwa uangalifu bila mapendeleo.

Pia napendekeza ya kwamba nafasi zozote za kazi zikitokea, kila wilaya nchini ipatiwe nafasi yake kiwaziwazi ili tuweze kupunguza umaskini na ukosefu wa kazi kwa nchi nzima.

Pia napendekeza ili kumaliza umaskini, katiba mpya na sheria za nchi ziwe ni kwamba kila wilaya ianshishe mradi

inayosimamiwa na serikali, na hasa miradi ya kilimo ili nchi isipungukiwe na chakula na tuwe na nguvu ya kulisha wananchi wetu.

Sehemu ambazo zina mito zinazotiririka, wilaya hizo zipatiwe project za kilimo. Kuwe ni lazima kuwe na project kilimo ili jambo hili lizuie wananchi waache kumiminika mijini wakitafuta kazi au nchi hii iwe na vyakula vya kutosha na pia kupatia wananchi kipato.

Kuhusu kilimo, ninapendekeza kuwe na sheria kwamba kila wilaya iwe na Quota ya Cereal Board kununua kiasi fulani. Serikali iwe ikinunua kiasi fulani kutoka kila sehemu. Nikitoa mfano kama vile Mwingi, tunakuza hapa mahindi na hata mawe, mtama na kunde. Kuwe kiasi fulani hata kama kuna ile serikali haitanunua kuwe ni lazima ili watu wapate soko kidogo.

**Com. Bishop Njoroge:** Taja jambo lako la mwisho.

**Benson Mutio:** Pia ni elimu. Ninazungumzia elimu. Sehemu hii kwa vile ina ukame na umaskini nyingi kama sehemu zile kame, kuwe na kiasi fulani serikali inalipia watoto wale wanapita kwenda shule za juu. Iwalipie fees, wasitoe fees. Hasa wale wanatoka jamii maskini, walipiwe mpaka vyuo vikuu kwa sababu sehemu zingine kuna umaskini.

Nikimalizia, ni upande wa chokoraa. Wale watoto wanaotangatanga kuwe na sheria kamili ya kutunza hawa watoto. Kuwe na sheria ya kuwajengea shule na kuwaokota wote na kuwapeleka huko ili watunzwe wawe raia wema kwa sababu wamekuwa ndio chanzo cha wakora.

Kuhusu hospitali, napendekeza ya kwamba vituo vyote vya afya vikimalizwa na wananchi, iwe ni lazima vifugnuliwe na serikali. Sheria ya namna hiyo itungwe. Kitu kingine, kuwe na sheria ya kuwakataza madaktari kufungua clinic sehemu wanahudumu kwa sababu jambo hili linachangia maovu. Kuweko na sheria ya kuwazuia.

Kuhusu kilimo nitasema kitu kidogo.

**Com. Bishop Njoroge:** Sasa sikia. Unajua ni lazima tufuate mpango fulani. Umezungumza mambo manne na nilikuwa nimekupa moja. Sasa zungumza ya mwisho.

**Benson Mutio:** Ya mwisho ni kwamba ile miradi itakayoanshishwa, wale watu watakaosimamia hayo miradi, wakae huko kwenye hayo miradi na wapewe mishahara ile ya juu na wawe na agreement na serikali na wakikosea, kitu cha kwanza ni kufungwa kwa sababu mtu kama huyo ameabisha nchi.

Apatiwe ile mshara ya juu kabisa na akae kwa ule mradi. Pale ndani. Akikosea awe mtu wa kufungwa jela.

**Com: Bishop Njoroge:** Asante sana. Utajiandikisha hapo. David Muoka? Francis Muthoka? Japheth Ndengi. Please

tuambiwe jina lako.

**Japheth Ndengi:** Hamjambo wananchi. Jina langu ni Japheth Ndengi kutoka Migwani. Sasa maoni yangu ningependa hii katiba tunafanya leo tuwangalie kwani kuna ma councilor ambao wana umri ambao imepita ile tunasema. Mtu hata kama ana miaka themanini hataki kutoka kwa kazi vijana wafanye kazi. Kuna macouncillor ambao wamekuwa miaka thelathini kwa kazi. Hao ndio wanafaa kutoka nao vijana sababu kazi imekosekana Kenya, hawa vijana waingie kule.

(Laughter)

Hiyo ni kitu moja ambayo tunataka mwandike hapo katika katiba.

Pendekezo langu tunataka councilor kama amechaguliwa akae miaka kumi. Asipitishie hapo.

Maoni ingine yangu ninaomba hii katiba mnafanya leo muende mkae chini kama vile mnakaa, muangalie chakula, mkague chakula kama iko sawa. Sababu gani? sisi mwingi tuna minister mmoja kule na akienda safari tunakaa bila minister na kuna sehemu zingine District kama hii yetu kuna ministers kama wawili. Mkae mwangalie chakula hii ya maministers mtuongezee mwingine au mtuonezee wabunge wengine. Sina mengi. Nimefikia hapo.

(Laughter and Applause)

**Com. Bishop Njoroge:** Asante sana Japheth. Catholic church syanda? Alex Musili?

Maingi K.N?

**Maingi Ngundu:** Kwa majina ni Maingi Ngundu na haya ndio maoni yangu.

The constitution should address clearly about the public lands. It should not be said that Public land outside Nairobi should be entrusted to the government by the county councils. Hii ni kumaanisha watu tupewe haki ya kumiliki mashamba yetu na kama ni kitu fulani hata kama ni dhahabu itapatikana kwangu, kama ni kuhamishwa kuwe na conditions ya kuhamishwa na kile nitapewa.

Number two: Sisi kama electorate tunatakiwa tupewe haki yetu. Kama ni sitting MP au ni Councillor tunaona hatutosheleshi, tunafaa kupewa jukumu ya kumwondoa.

Number three: Our courts. Koti zetu pia sheria inafaa ieleze vizuri kwamba ike lugha inatumiwa kule wananchi wengi hawaiielewi, kwa hivyo inafaa tuelewe, koti zetu ziwe na lugha tunayoelewa na pia hukumu ya kifo ningefurahia kama ingeondolewa.

Point number four. The constitution should also address the family planning issues. Most people should be allowed to have two children and if need be for a third one, they should apply to the government.

(Laughter)

My point number four is about the provincial Administration. I think the provincial administration especially here in our Country is consuming a lot of money and at the same time giving little service to the citizens. I would wish the constitution said that the only position in Provincial administration that helps Kenyans is the position of a Chief or an Assistant Chief. All the other capacities of the Dos, DCs and PCs actually have no duty they are doing to us, they are eating a lot of our good money yet we don't have much money in Kenya.

For example I in particular am over twenty years and I have never received any service from the DO to the PC. This people are eating a lot of money and doing no job. I wish those posts we scrapped in Kenya. Let us have chiefs who are answerable to the community. A chief who is a government official and is answerable to the community. The community be given exactly that chance. If you want to eliminate the person and the same time unaweka mwingine because these people and especially in ukambani they have very outlived. Some of them are known to be good campaigners; they were recruited because he was once a teacher and when he opted to campaigning he was made a chief. It is we people who should be given that chance. Thank you.

**Com. Bishop Njoroge:** Watu wengi wamesema kwamba kama MP hawafanyii kazi, au Councilor, waondolewe kabla ya kipindi chao na wananchi. Ni njia gani itatumiwa? Mngetaka tuweke nini kama kiwango kama MP hafanyi aondolewe?

**Japheth Ndengi:** Mimi nilikuwa na maoni kwamba kuwe na Committee ya wazee fulani. Those wazee kama kumi kwa constituency ambao wanajulikana, those known to be good. They should not be political people. Siyo wale wanasiasa wazuri. No. Wazee wale wanaaminika. Sisi kama Wakamba tunawajua wale wazee wa Kikamba wazuri. So wakichaguliwa nao pia watoe sababu mzuri si kusema mbunge fulani ni mbaya na hawatoi sababu. There should be good reasons as to why ni mbaya.

(Applause)

**Com: Bishop Njoroge:** Umesikia umepigiwa makofi. Mary K. Kamwara? Otieno ?

**Peter Kalii:** Jina langu ni Peter Kalii na kwangu ni hapa Mwingi. Mapendekezo yangu ni kwamba katiba itengeneswe iwe na language moja ya kiswahili iliyo lugha ya taifa.



Na pia katiba itengenezwe ambayo itafanya kila mtu awe na haki ya uhai, kujieleza, kuungana na watu wengine, matibabu ya bure, elimu ya bure, mtu awe na mahali pa kukaa na awe na haki ya kujieleza.

Pia nataka katiba ipige marufuku mtu mmoja kuwa akipatiwa mshahara mara mbili; yaani mtu mmoja awe na mshahara moja.

Pia ninauliza katiba katiba I-split Public Administration iingie katika ministries zingine.

Pia nataka katiba impe kila mtu uwezo kwa wafanyi kazi wa serikali wote, wakiandikwa wawe wanaonyesha ujuzi wa kazi ile ambayo wanafanya; walioandikiwa.

Pia ninauliza katika katiba iwekwe commission ya complaints ambako mtu yeyote akionewa anaweza kupeleka malalamiko yake halafu ichunguzwe.

Pia ninauliza katiba serikali kuu ipatie serikali za wilaya madaraka ya kuendesha kazi kama agriculture, kama macourt na hata kama maji pamoja na energy.

Pia nauliza Judicature ipinduliwe; sheria za mahakama zipinduliwe ili watu wawili wakisikizana wafanye mahakama nje ya koti, wazee wakisikizana, hiyo iweni mahakama.

Pia ninauliza katika katiba kuwa yote ya watu wa Kenya ambayo ilipelekwa nje, irudishwe hapa.

Pia nauliza katika katiba, mtu yeyote akitaka kiti chochote cha kuchaguliwa, awe akichunguswa alikotoa hiyo mali. Ni hayo tu.

**Com. Bishop Njoroge:** Asante sana Mzee. Njoo hapa, hayo ni maoni mazuri. Sasa ninataka kumpatia waziri nafasi naye aweze kutupatia maoni yake. Karibu Minister.

**Hon. Kalonzo Musyoka:** Asanteni sana Commissioners na ningeomba radhi kwa kuwa nimekuja kama nimechelewa na ingekuwa ni mapenzi yangu kuwa nanyi tangu jana. Naelewa kuwa mlikuwa na kikao kama hiki upande wa Seikuru Secondary School na vile vile Kisu Secondary School na hiki ndicho kikao cha tatu na cha mwisho.

Hamu yangu haswa ni kuwasikiliza ninaowawakilisha bungeni wakitoa mawaidha yao na kwa hivyo mimi nitajaribu nijifiche sana nisije wenzangu hapa wakasema yale mheshimiwa amesema ndiyo hayo kwa sababu ningetaka yote myasikize kutoka kwa wananchi. Kama ambavyo mnajua kama member wa kamati ya bunge ambayo inahusika nanyi, nitakuwa na fursa bila shaka ya kutoa mawaidha lakini kwa sababu niko hapa nyumbani, ningetaka niseme moja, pengine mawili. Pengine yote hayatawekwa kwenye katiba directly lakini mtasikiza yale yanaoyotukera sisi kama wananchi wa Kenya wanaoishi sehemu hii.

Ningetaka niseme hivi; Kwanza kwamba tuko na katiba na katiba ambayo tunajaribu kuiunda upya inatokana na katiba ambayo imekuwa nasi tangu wakati ule wa sitini na moja from Lancaster House until now and we have seen amendments to that constitution and so it has served us well.

Havng said that, katiba haiwezi kuwa static; haiwezi ikasimama tu mahali pamoja kwani mahitaji ya wananchi inaweza ikaongezeka vile kiwango cha wananchi wenyewe kimekuwa kikiongezeka na kwa hivyo hatuna budi ila kuangalia ni yapi tunaweza tukafanya.

Kwa hivyo sisi kama wakaaji wa sehemu hii, taabu ambayo tuko nayo haswa ni katika ugawaji wa usawa wa mali ya asili ama national wealth. Unequal distribution of national wealth. Tunaona ya kwamba sasa hivi kwa mfano mimi nililala upande wa Aberdares; Tree Tops, nikapata chai Nyeri. Nikapitia Kirinyaga, naona kule wanapanda majani chai, wanamashamba masafi sana, hewa ni tofauti ikilinganishwa na hii yetu huku, huku kuna jua kali. Nikapitia pia Embu, na kwa hivyo unapata kwamba mpango ulioanzishwa na serikali wa DDC was ---? meant.

I think now in terms of distribution of national income we have to have some inbuilt mechanism within the new constitution ambayo inahakikisha usawa wa ugawaji wa mali ya taifa ili sehemu kama hizi ziweze pia kufaidika bila ku-sweat sana. Mimi kama mbunge hata kuja kupatiwa wilaya kama hii na Rais wengine walikuwa wakipiga kelele wakisema this is a political district na najua kwamba tangu jana mtaona kwamba mlianza mbali, na hii ni constituency moja. Ilikuwa wakati mmoja mimi na Mheshimiwa musila. Alikuwa my voter. Vile vile mheshimiwa Nyenze was my voter because people living in Nairobi hawajui shida walizonazo wananchi kutoka sehemu ambazo ni kame kama hizi.

So semi-arid areas in particular, we need special attention katika katiba mpya. I am suggesting therefore that we give strength to local authorities. Strengthen kabisa kabisa ili kwamba ikiwa ni macouncillor wawe na officers ambao ni competent, wenye ujuzi ambao wataweza kuleta manufaa kwa wananchi. Therefore na ikiwa inaonekana pengine there is a current thought ya kwamba na tukifanya hivyo na mali ikiwa inaweza kutoka a through local authorities kuja directly kwa wananchi wanaohusika, utapata kwamba pengine kutakuwa na usawa.

Najua kwamba wenzangu wamezugnumzia swala hilo kusema wapatiwe mamlaka fulani fulani. They were talking about devolution of power. Devolution I think is what we want to see.

Swala muhimu kabisa whether to go federal or not, nimepitia pale nikaona Dam yetu inaitwa Kamburu na next to it is Kindaruma. Katika Province hii the only natural, what we would say is our contribution to national wealth may be is this generating capacity wa mto wetu huu wa Tana na Athi River. I know that if we strengthened local Authority tutakuwa na uwezo wa ku-generate faster wealth kwa watu wetu.

Rasilmali therefore is another angle. Kama mbunge wa hapa vilevile, nikiangalia mimi macommissioner, naweza nikasema kuwa sehemu tunawakilisha bungeni ni kubwa sana. Ofcourse we cannot say ---? that Mwingi gets another two MPs, it has got to be written within the constitution. Nimekuwa juzi na wabunge wa Assembly ya Afrika ya Mashariki ambayo imetokana na jumuiya mpya ya eneo letu hili na nikaona kwamba nchi kama Uganda na Tanzania wana wabunge wengi kishinda Kenya na hali population ya Kenya na Tanzania ni karibu sawa. Kuna umuhimu kwa mfano District kama Mwingi hii ili kujaribu kutatua shida za wananchi, kuwe na wabunge ambao wanastahili. Siyo kuangalia idadi tuseme a hundred thousand.

Nimesikia people saying a constituency iwe na wakaaji elfu mia moja. Utapata kwamba if we follow that route alone without taking into account the particular geographical features of every locality, there will be injustice being worked on a number of our areas and this one in particular because in my view we do require not less five members of parliament in order to be able to deliver services effectively kwa wananchi.

Therefore we need then, I don't know tutalegislata kwamba tuwe na wabunge minimum figure three hundred thousand but I think what we can do is come up with a formula. Wakati tuna kuja na formula kama hiyo tuangalie tusije tukasema tu ni mahali ambapo kuna na watu elfu mia moja ndipo wanapata kuwa na mjumbe kwa sababu tutakuwa tumewaonea walio wengi ambao wanaishi katika sehemu ambazo si sawa na mahali ambapo wengi because of geography and rutuba ambayo iko for example the Mount Kenya Region. You find a concentration of our people there na huku pia kuna wananchi wakaaji .

Ofcourse at the end of the day tungetaka pia area kama hizi kuwe na ongezeko la mikoa. Sasa hivi tuko na mikoa saba and because we are talking devolution, we may have to consider kuwe pia na mkoa mwignine katika Eastern Province. Kwa hivyo ukiangalia kutoka Marsabit, Moyale, mpaka wa Ethiopia mpaka Tsavo national park, hiyo ni dunia nzima. We think that, just like am sure watu wa Rift Valley will speak for themselves in terms of North Rift and South Rift, vile vile Eastern Province is so large na tunahitaji vile vile Pengine kuwa na mkoa mwigine ili kuwe na usawa as we think of devolution, preparing ourselves for that eventuality.

Pia ningetaka kusema kwamba mengine ningetaka kuzungumza katika kumbukumbu maalum ambayo itatolewa na chama cha KANU. We are finalizing our positin and as soon as that position is clear, vitu kama the spread of presidential powers ambayo imezungumza na wengi.... Ofcourse everybody anakubali, KANU included, that we need to spread the Presidential Powers, to have an Executive President, to have a Vice-President, vile vile kuwe na Prime Minister na two Deputy Prime ministers. Tunazungumza kama chama na tunaona kwa kuna usawa na vile vile if a President has to have a Vice-President as a running mate, as soon as they are elected, then they can relinquish their positions. I don't know, am not very clear what should happen to the Prime Minister because huyu pia atachaguliwa na wabunge, hawezi akachaguliwa directly. So, this is a way we are looking at it.

Vile vile kuwe na Supreme Court in order to enhance the level of delivery of services in that area; dispensation of justice kwa sababu twaamini kama chama kwamba justice must not only be done but must manifestly be seen to be done in all cases. Na kwamba justice delayed vile vile is justice denied. Kwa hivyo utapata kwamba ukienda kwa koti zetu kunarundikana kesi na ndio maana unasikia wengine wakisema pengine turudi kwa wazee. Kesi ni nyingi sana. We need to do something and this is why we are thinking of a Supreme Court and ofcourse addressing the question of the necessary jurisdiction kwa mambo kama hayo.

I was very clear on the need to strengthen the local authorities. This is what will help us. Hii ndio itawasaidia sana wananchi kila mahali and so kwa sasa ningetaka nikome hapo. I know you are under pressure to listen to many people. Sitaki nichukue nafasi moja zaidi. Ningetaka niwaachie wananchi wenyewe wazungumze, nimewasikia wengine wakizungumza na kila mtu anatoa akili yake, vile anavyoona mwenyewe. Hata kama anaongea lugha gani, najua kwamba tunaelewana at the end of the day. Wengine wako na vitina zao; ikiwa mtu anaweza kupigana na Rais wa nchi kwamba akitembea ni makosa.

I can tell you that we have in this Country a President ambaye, and it is not usual in Africa, anatembelea watu wake. This is what Kenyans need. Kutembea na kujua shida za wananchi and that is the kind of leader we have today. I think the next leader will have a big problem ikiwa haezi akafuata mtindo huo. Akikaa kwa ofisi kama vile wengine wanavyofikiria.

Atafukuswa na wananchi kwa sababu nimesikia wanataka laws relating to impeachment ya wabunge na wengine na wengine lakini nafurahia kijana ambaye amezugnumza juu ya kuwa na wazee. Wazee ambao wanaangalia kila mahali. Kama tungekuwa namna hiyo nadhani kwamba nchi tutazidi kwa sawa sawa lakini tumshukuru mungu kwamba ametufikisha kiwango hiki.

As I said, constitution making has to be a continous process. Mengine nitazungumza pengine na watu wa press niwajibu watu wa Nairobi, nikitoka katika kikao hiki. Tena mjihisi kwamba mko nyumbani kwani nyinyi bila shaka mko nyumbani kwani nyinyi bila shaka mnaelewa kila sehemu ya nchi ni sehemu yenu and I know you have to struggle very hard to beat certain deadlines. Kwa hivyo tutajaribu tuwazaidie vile tunaweza katika kutoa mawaidha yaliyo sawa. Asanteni.

(Applause)

**Com. Bishop Njoroge:** Asante sana. Tuna jambo moja au mawili.

**Com. Zein:** The Hon. Minister thank you for your views. I think we had clarified the issue of constituency representation in terms of balancing the population and the geographical coverage. What I would like to, possibly not now but later own, prick your brains on is the issue of creation of new Provinces and re-drawing boundaries.

I was one of the Commissioners who was in Taita Taveta District and one of the views, some of the views we got from the

people is that you need to re-draw boundaries but our border goes up to Mtito Andei. This is what people were saying in in Taita and you just mentioned Tsavo national park; that Eastern Province goes up to the park. So then, I think there will be a point where we will need to sit down and talk about that.

**Hon. Musyoka:** Thank You. I know that the issue of boundaries is necessarily of necessity a very sensitive matter. Juzi jirani zetu hapa Tana River walikuwa na mkutano mahali panaitwa Ukasi within Mwingi District na councillor mmoja wa upande wa Tana River akasema Seikuru, mahali mlikuwa jana, is supposed to be in Tana River District. Hebu fikiria. Hiyo ni kumaanisha mjumbe wa Mwingi North is here illegally, angekuwa upande ule mwignine. I think it is fairly sensitive.

What I think we are saying is looking at the issue globally and we do recognize that there is need; there is need if we are going to really go down to our people and address the question of infrastructure building.

Utaona kwamba, kwa mfano hapa Mwingi, one of our dream projects is really to have the road from Mombasa not going through Nairobi but coming through Kitui, Mwingi, Maua, Archers Post, Isiolo. That is the shortest route to Ethiopia, believe it or not, and can you imagine what that would mean if we had a properly tarmacked road. Ethiopia is today land locked and they would want to use to access our port of Mombasa.

And similarly if you look at it that we do need at least a dual carriage way between Nairobi and Mombasa, and beyond from Mombasa to a border with Malava in Uganda, if these things were possible, am talking infrastructure here, you need to be able to empower people who can take quick decisions and this is why the need to devolve is so urgent because some of our central planners sitting at the ministry headquarters are not able to appreciate what I have just told you.

Ukimweleza Pengine hata katibu mkuu mzima hawezi akaelewa ni kitu gani ambacho nimekitaja, and they know about the Kapiti, they keep on talking about them and you find that local authorities infact should have power to go out there and source funding.

That way we will be able to generate more wealth for this country, there will be a lot of economic mobility as well because what is happening is as I was coming nilikuwa nikifikiria jameni kama kungekuwa na train service kutoka hapa kwenda Nyeri kwa mfano because it is very short unakata tu kupita upande hiyo but this cannot be addressed unless we seriously address the question of devolution.

This is what the KANU has been able to recognize and we are looking at it. Devolution of powers to the local authorities lakini in re-drawing provincial boundaries, I think we should be careful not to open the pandoras box then we end up with a situation where endlessly mnakaa na wazee, mnaenda kotini including the supreme court because I can tell you hawa wakiwauliza hawa wakamba wanaishi hapa in their view pengine boundary ya Tana River ingekuwa hii barabara ya kwenda Garissa because all

the names in Kora National Park, Mwingi National reserve huko ndani, Mwingi national reserve is of course Mwingi lakini ukiingia Kora utaingia majina kama Kalimangilu, majina ya ukambani, but they are in Tana River District. Na tunajua kwamba ukiyaguza sasa hivi, you are courting a lot of concern. I think it is possible to agree easily to on atleast addition of two provinces as we go ahead. It is quite possible. Thank you.

**Com. Bishop Njoroge:** Mimi pia nilikuwa Marsabit na nilikuwa eneo hizo na kila mahali tulienda walisema wangetaka kuwa mkoa wao. Kwa hivyo tungependa mfikirie kama mkoa huu tukiwa na mkoa mwingine, itaweza kuchukua District ngapi na zitafikia wapi na mpaka utakuwa wapi? Kwa sababu imefikia watu wa District hizo wanataka mkoa wao na ninajua kuna shida kwa ajili ya labda ya Isiolo na nini kwa hivyo hii ni mambo ni lazima tuyafikirie kwa sababu tusipoyatatua sasa....

**Hon. Musyoka:** Eastern Province Commissioner is in three parts basically: Moyale, Isiolo, Marsabit; we do not do that. That is one part of this province. Infact we do have eight communities. Kunayo moja ambayo hata inatangaza mambo yao na lugha yao inayoitwa Burch; not many people know about the Burchis. They have every right to belong to this Country. Therefore the constitution must take into account the need to safeguard interests of even the smallest communities. This is what will keep us going.

Kwa hivyo wakitaja kwamba wanahitaji mkoa wao, it is out of the practical realization that Eastern Province is actually in three parts: The Northern Part, the Mount Kenya region and ofcourse the southern part which is mainly the four Districts of Ukambani. It may make a lot of sense to think in terms of three provinces because that way will bring faster development to this province and ofcourse to this Country.

Ofcourse I said that may be in my view; this is rule of the thumb; we do require not less than three hundred members of parliament in this Country, globally. From the present two hundred and ten constituencies, we do need to create another ninety constituencies in order to make it possible for our people to get faster services. Thank you.

**Com. Bishop Njoroge:** One last point: Where we were yesterday, the people were talking about title deeds. Although it could be a constitutional issue, it is very much also an administrative issue. I don't know whether you have given thought to this.

**Hon. Musyoka:** I have and am actually very concerned myself because utapata kwamba the process should have gone faster had it been that if you declare an area, an adjudication, utapata kwamba kila mtu anaanza ku-claim hapa, cases zinaanza, wazee wanaanza na taabu moja tumekuwa nayo hapa ni, I have nothing against wazee lakini utapata kwamba the richer person ndiye anaenda, ikiwa wazee wanakutana chini ya chairmanship ya D.O, ama chief kujaribu kutatua cases kama haya ya ardi, inachukua muda mrefu kabisa until the Minister has to appoint special DCs to adjudicate on this matter. In the process ni kwamba we are seriously disposed in this area because we do not have title deeds.

In my own constituency I think I do not know anybody with a title deed; so this is how serious it is. And ofcourse we have been urging the minister of lands and settlement. Watasema wakati mwingine, this is why devolution is important. Imagine if the county councils were able to move on their own; hatungekuwa na taabu lakini wengine watasema films zimeisha; I can tell you there are many times we have been able to talk with our colleagues in the ministry of local government, unapata ya kwamba title deeds hazitoki and so these people cannot go to a bank and borrow money.

Sasa naona Kenya Commercia Bank hapa kazi yake ni kukusanya pesa kutoka kwetu kwa sababu sisi ni wafugaji kwa upande mwingine. Wale ng'ombe tunauza tunaweka account hapa zinachukuliwa zinapelekwa Kenya Commercial Bank headquarters Nairobi and then others borrow pesa zetu na sisi wenyewe hatuna benetits.

Kwa hivyo unapata ya kwamba jambo hilo linazidisha umaskini na umaskini ni kitu tumeapa na tumeamua kupigana nao. Thank you.

Com: Bishop Njoroge: Bwana Minister, I think you will go there to the Programme officer and have your details taken.

**Hon. Musyoka:** I had registered there, do you want me to register again?

Com. Bishop Njoroge: Yes. Okay. Linner Munyoki? F. N. Maithya? Tafadhali njoo hapa mbele. Ningetaka kuwajulisha, kwa sababu kuna watu wakuja sasa hivi, sisi ni Commissioners kutoka huko Nairobi. Huyu anaitwa Abubakar Zein na mimi naitwa Bishop Bernard Njoroge, ili muweze kutujua. Asante.

F. Maithya: Asante sana bwana mwenyekiti. Maoni yangu kabla sijayasema, nitataja jina langu. Jina langu ni Fredrick Kaluki Maithya kutoka sub-location ya Kaliteti, hapa Mwingi.

Maoni yangu ni machache sana. Katiba ambayo tutakuwa nayo, naomba serikali yetu tuwe na waziri mkuu na mdogo wake. Tuwe na president na mdogo wake; na hawa watu wote tuwachague kwa kura.

Electoral Commission tuwe na Commissioners wawili kutoka kila Wilaya. Mmoja mkubwa na mdogo wake.

Councillor tumchague na kura.

Ingingine: Naomba katiba yetu itusaidie kwa sababu tunapoteza ngo'mbe wetu wengi sana. Kwa mfano hii barabara ya kutoka Garissa kwenda Nairobi ina lori nyingi sana na hizo lori zinapitia ng'ombe wetu juu na wanaisha wote na huku mwempe lori anakutafuta wewe mwenye lori utengeneze lori yake. Hana haja na ng'ombe wako. Hata wewe mwenye ngo'mb unaanza kukimbia ndiyo usishikwe, upeklekwe polisi, ulazimishwe kutengeneza hiyo gari. Kama inawezekana, katiba yetu ijaribu hata kama ni ngo'mbe mbili wanagongwa, nilipwe moja badala ya kuambiwa siwezi lipwa wote. Mnajua sisi ni wafugaji.

Ingene: Hapa Mwingi tunao MPs wawili; mmoja ni minister. Hii ni District kubwa sana. Kama wewe bwana mwenyekiti umeshaizunguka. Hatuwezi tukapatiwa MP wa west na tukapatiwa MP wa central na MP wa East? Kwa sasa tuna MP wa South na North, hatuna wa Central.

Sina mengi, yangu ni hayo. Asanteni.

Com. Bishop Njoroge: Tungetaka kumsikia W.Martha Simon.

W.Martha Simon: Asanteni. Jina langu ni Winny Martha Simon. Ningetaka kuuliza katiba, ikiwa itaweza, iturekebishie sisi wanawake maana tumeteswa sana na wanaume wetu waliotoroka manyumbani. Sana sana kurudi kwao ni kwa vishindo na hatujui ni wapi ambapo tutaweza kupeleka malalamiko yetu. Ningeomba katiba itafute amri au ichukue hatua kwa yeyote; awe mke au mume aliyetaka kurudi nyumbani na alikuwa ametoroka kwa miaka kadhaa, aje pole pole. La si hivyo, achuguliwe hatua kali.

Jambo la pili ningetaka ikiwa hawezi kija kwa utaratibu, hatua ichukuliwe na ikiwani kufungwa, afungwe afunzwe adabu ya kuingia nyumbani kwake. Hakatazwi kwake.

Jambo la pili: Sisi wanawake tumeonekana kama sio watu wa maana sana lakini kwa kuwa tumekaa manyumbani, tunajisikia kama sisi ndio wenye nyumba na tungetakasisi tunaokaa nyumbani pamoja na watoto, tuwe na uridhi wa mali yetu. Hata ikiwa mtoto yuko na miaka miwili, awe na uridhi na ardhi yake; hata ikiwa ni ya robo acre. Hiyo ni kuonyesha hatutaki kuweco na tofauti kati ya mtoto wa kike na yule wa kiume.

Jambo la tatu: Sisi wanawake tunaokaa nyumbani sana sana tuko mbali sana na maji, na barabara vile yalivyo sasa, hasa hizi zilizo na lami, tunateswa sana maana tunaona bumps tukifika town. Tunataka kila barabara ndogo ikitokea kwa main road tuwe na bumps ili zile gari zipunguze kasi na sisi na watoto wetu turudi barabarani kwa utaratibu.

Jambo la nne: Wakati wa njaa ukiingia, sisi kina mama tunateseka sana na tukioa, tunapatiwa chakula wakati wa malisho. Ile chakula ya msaada. Utaona tuing'ang'ana sisi na watoto, mama na hata wazee. Twataka tujue, hii haki ya chakula ya jikoni ni ya Mzee au ni ya mama watoto? Maana wazee wengine wakichukua hiyo chakula haifiki nyumbani. Twataka hiyo chakula iwe ikipeanwa kwa wanawake tupu na ikiwa ni mwa naume, awe hana bibi na hana mtu wa kuwashughulikia watoto wake.

(Laughter)

Jambo la tano: Sisi wanawake wa nyumbani, kazi yetu ni kulima. Hospitali tunapata kwa shida. Tukienda hospitali unaambiwa



ununue kadi, kuandikiwa ni pesa, dawa ni pesa, kumwona daktari pia ni pesa. Twataka katiba ituangalie vizuri. Je, tutakaa tukiteseka mpaka lini? Na ikiwa tutapumsika, tutapumsika mwaka gani? na ni wakati gani? Hivi sasa tunangoja kupumzika. Twajihisi tuko huru, lakini kulingana na tunavyoteseka, hatuhisi uhuru wetu. Tunajihisi tungali wafungwa.

Jambo la sita: Watoto wanatafuta kazi na ile kazi hawaipati. Je, ikiwa kuna msaada ya watoto hasa youth, awe msichana au mvulana, utolewe kwa kampuni au mfano wa jambo la kuwatafutia kazi ili wapate kazi maana wasipopata kazi, wengine watajipatia magonjwa ya zinaa, wengine wawe wezi na kila aina. Kwa hivyo wakiendelea hivyo tutawakosa watoto. Yule bwana anayekaa town akirudi nyumbani hatawakuta watoto. Kuna njaa na watoto wamekwenda kujitafutia na ni kwa ajili ya matatizo. Katiba ituangalie sisi kina mama ili tukae nyumbani kwa utaratibu na uvumilivu. Maneno yangu ni hayo. Asante.

**Com: Bishop Njoroge:** Asante sana mama. Hayo tumeyasikia na tumeyaandika. Karibu hapo kwa.... Tungetaka tumpate K. Dorcas. K. Dorcas yuko? Tumpate mama mwingine: Rose Mulungi. Unaitwa nani?

(Response Inaudible)

**Com. Bishop Njoroge:** Sijakuita na hauwezi kuleta kwa niaba ya mama. Mwache ajiseme. Ni bibi Yako?

**Rose Mulungi:** Hapana. Kwa jina naitwa Rose Mulyungi na nina maoni kuhusu katiba. La kwanza ni juu ya no discrimination: Kina mama, ingawa Section 22 of the Constitution forbids all forms of discrimination, often the law implicitly tends to allow the discrimination against women on the basis of sex. It has encouraged discriminatory laws dealing with property, land and child custody. That happens through many ways.

